

Je unaujua ufunguo wa wewe kumpenda Bwana zaidi?.. kuna jambo ukilifanya basi upendo wako kwa MUNGU utaongezeka kwa kiwango kikubwa sana.. Utajikuta unampenda MUNGU zaidi, unamheshimu zaidi na unamtumikia zaidi.

Na ufunguo huo si mwingine zaidi ya kuutafakari MSAMAHA WAKE KWAKO KWA MAPANA!.. Unaweza kuona jambo la msamaha kwako ni dogo tu!.. Lakini nataka nikuambie Msamaha wa MUNGU kwako una uhusiano mkubwa sana na UPENDO WAKO KWAKE!.

Maandiko yanasema “aliyesamehewa sana hupenda sana, na aliyesamehewa kidogo hupenda kidogo”

Luka 7:47 “Kwa ajili ya hayo nakuambia, Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi kwa kuwa amependa sana; lakini asamehewaye kidogo, huyo hupenda kidogo”.

Hebu tafakari huu mfano: Mtu mmoja alikuwa anadaiwa shilingi 500 na mwenzake na akasamehewa na mwingine alikuwa anadaiwa shilingi laki 5 na mtu huyo huyo mmoja, naye pia akasamehewa kiasi chote cha pesa (*shilingi laki 5*)..

Je yupi kati ya hao wadaiwa wawili waliosamehewa, atampenda zaidi Yule aliyewasamehe?.. Bila shaka Yule aliyesamehewa deni kubwa ndiye atakayempenda zaidi aliyemsamehe, na hata kumheshimu sana..

Lakini Yule aliyesamehewa deni dogo, anaweza kuwa mtu wa shukrani lakini si katika kiwango kikubwa, na wala hawezi kutoa heshima ya kiwango kikubwa kwa yule aliyemsamehe.

Ni hivyo hivyo katika upande wa Imani, watu waliojiona ni wenye dhambi nyingi na kubwa kubwa!, na kujiona kama hawajastahili msamaha kwa makosa yao, wanapoungama na kupokea msamaha, huwa wanampenda sana Bwana YESU na kumheshimu.

Lakini watu wanaojiona ni wasafi au watakatifu sana, kwamba hawamkosei sana MUNGU huwa hata upendo na MUNGU hawana, au upo kwa kiwango kidogo.

Sasa kiuhalisia wote tumemkosea MUNGU pakubwa sana!.. ukijiona huna dhambi nyingi, basi fahamu kuwa kuna shida kwako ya kutafakari, ambayo hiyo sasa ndio unapaswa ushughulike nayo.

Unapaswa ushughulike na hiyo hali mpaka ifikie hatua ujijue kuwa hukustahili, na wewe ulikuwa ni mbaya mno, na mbovu, na makosa yako

yalikuwa makubwa sana!.. ukiweza kufikia hiyo tafakari, basi jua matunda yako ni wewe kumpenda BWANA na kumheshimu sana.

Unawezekana wewe sio mwizi, au muuaji au mzinzi lakini hebu tafakari vipindi ulivyomsema ndugu yako, na MUNGU alikufumbia macho, ingawa ulistahili adhabu ya mauti papo kwa hapo.

Hebu tafakari vipindi ulivyotamani vitu visivyofaa moyoni mwako, na MUNGU alikufumbia macho ingawa ulistahili kufa papo kwa hapo.

Hebu tafakari vipindi ulivyokasirika bila sababu, tafakari vipindi ulivyokuwa unawaza mawazo mabaya, tafakari vipindi ulivyodanganya na kusema uongo, tafakari vipindi miguu yako ilipokuwa inaelekea kufanya maovu, tafakari vipindi ulivyotukana mdomoni na moyoni mwako, tafakari mambo ya upumbavu uliyoyafanya mitandaoni, hayo yote si kwamba MUNGU alikuwa haoni, au hata sasa hayaoni, anayaona yote!.

Inawezekana hujawahi kuuu, lakini tafakari vipindi ulivyokuwa mbinafsi, tafakari visasi na vinyongo ulivyokuwa navyo, na huenda unavyo hata sasa, tafakari udunia wote ulioufanya, rudi nyuma kumbuka tukio moja baada ya lingine katika maisha yako, yatakafari sana halafu fikiri YESU AMEJITWIKWA makosa yako yote hayo, ambayo kama si rehema zake

huenda ungekuwa umeshakufa na upo KUZIMU sasa!.

Lakini alikizuia kifo kisikupate!, umempa nini?, au una umaalumu gani hata akusamehe hayo yote?, kwani waliokufa bila kupata huu msamaha wana kasoro gani zaidi yako?.

Je huoni kama aliyekupa huu msamaha ni wa thamani kubwa? Huoni kama amekusamehe makubwa sana.. bado humpendi tu!.. ungepaswa uwe kuzimu muda huu, lakini bado unaishi! Bado kwako unamwona vile vile?

Ndugu tenga muda sana utafakari msamaha wa YESU, kwani ndio uliobeba funguo za kumpenda YESU zaidi, Ukiutafakari msamaha wa YESU utaishia kumpenda, lakini pia kumwogopa (*kutokutenda dhambi tena*)

Zaburi 130:4 "Bwana, kama Wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama?"

4 Lakini kwako kuna msamaha, Ili Wewe uogopwe".

Shalom.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

NGUVU YA MSAMAHA

UMUHIMU WA KUOMBA MSAMAHA.

NI KWA NAMNA GANI KRISTO ALIZIBEBA DHAMBI ZETU?

JE UMEUPOKEA UWEZA WOTE WA UUNGU NDANI YAKO?

Hadhari ni nini kibiblia? (Mithali 1:4)

Share on:
WhatsApp

Print this post